HABARI
**CPA MAKALA AWATOLEA UVIVU CHADEMA** Uk.2



**20 Mbaroni kwa kula mchana Mwezi Mtukufu wa Ramadhani** Uk. 4



**ALIYEPENDEKEZA JINA LA TANZANIA AFARIKI** Uk.2

Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvinews@gmail.com

GAZETI LAKO

# JAMVI LA HABARI

ISSN Na 2683 - 6548: Toleo Na. 2542 JUMATANO MACHI 05, 2025 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

# WAZIRI MAVUNDE AMWAGA FURSA SEKTA YA MADINI

- **Azikaribisha** sekta binafsi kushirikiana na serikali kutafiti madini
- **Serikali** yaahidi kuongeza eneo zaidi la kufanyia utafiti wa kina
- **Aileleza** STAMICO kufanikisha upatikanaji wa vifaa ya Utafiti kwa wachimbaji wadogo 777 Uk.4






## Dk. Biteko: Afrika ipo mbele kwa ajenda mabadiliko ya tabia nchi

Uk.3

# WAZIRI MAVUNDE AMWAGA FURSA SEKTA YA MADINI

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Madini Mh. Anthony Mavunde amezikaribisha nchini Tanzania Kampuni za Utafiti wa madini kushirikiana na serikali katika kutimiza malengo ya Mining VISION2030 ambayo imejikita katika kufanya utafiti wa kina wa madini kufikia eneo la ukubwa wa asilimia 50 kufikia mwaka 2030.

Mh. Mavunde ameyasema hayo jana Toronto, Canada wakati akihutubia kikao cha Mawaziri wa Madini kutoka nchi mbalimbali duniani,Kampuni za Utafiti na Uendelezaji Migodi na Asasi za kiraia.

ìSerikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia S. Hassan imeweka mazingira wezeshi ya kiuwekezaji,hivyo ni fursa kubwa ya Kampuni za Utafiti kuja kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika mkakati wake wa kuongeza eneo lililofanyiwa utafiti wa kina wa madin i.

Kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Madini, inatekeleza mpango wa utafiti wa madini wa kina kutoka eneo la utafiti wa kina la asilimia 16 kufikia eneo la asilimia 50 kufikia mwaka 2030.

Kwa kuwa Tanzania ni kisiwa cha amani, uongozi imara na mazingira mazuri ya kiuwekezaji nichukue fursa hii kuwakaribisha wadau kuungana na serikali katika mpango wake huu wa utafiti wa kina wa madini nchini kwa kuwa serikali peke yake haiwezi kufanya kwa eneo lote hivyo sekta binafsi ni muhimu katika kufikia azmaìAlisema Mavunde

Awali akiwa katika mabanda ya maonesho ya vifaa vya Madini,akiongozana na Balozi wa Tanzania nchini Canada Mh. Joseph Sokoine na wataalamu wa Wizara ya Madini,Waziri Mavunde amemuelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO Dkt. Venance Mwasse kuangalia namna ya upatikanaji wa vifaa vya utafiti wa awali wa madini ili wakati wachimbaji wadogo wakipata huduma ya uchorongaji kuwepo pia vifaa vya awali vya kusaidia kuonesha maeneo yanayopaswa kuchorongwa.



# CPA MAKALA AWATOLEA UVIVU CHADEMA

NA MWANDISHI WETU

KATIBU wa Uenezi na Mafunzo wa CCM CPA Amos Gabriel Makala alisema kuwa viongozi wa Chamdema kuanzia Mwenyekiti wao Tundu Lisu na wenzake wote, hakuna hata mmoja mwenye ubavu wa kuzuia kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu nchini hapo mwezi Oktoba mwaka huu.

Akizungumza katika mkutano wa viongozi wa chama na jumuiya ngazi ya shina, tawi, kata na wilaya katika Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es salaam CPA, Makalla amesema kuwa CHADEMA inafanya Makosa makubwa kuwahadaa wananchi wasijiandikishe kwa madai kuwa hakutakuwa na uchaguzi.

Amesisitiza kuwa uchaguzi utafanyika kwa mujibu wa sheria na katiba, na kwamba madai ya CHADEMA kwamba ìNo Reform, No Electionî ni propaganda zisizo na msingi na hivyo zipuuzwe.

Vilevile amewataka Wenyeviti wa Serikali za Mitaa waliochaguliwa katika uchaguzi uliofanyika Novemba Mwaka jana, kutanguliza huduma na utumishi kwa wananchi wao, kwani waliomba utumishi na wakiwakilishe chama kama walivyoaminiwa.

## ALIYEPENDEKEZA JINA LA TANZANIA AFARIKI

NA MWANDISHI WETU

MOHAMMED Iqbal, aliyekuwa msomi na mchambuzi wa masuala ya kisiasa, alikuwa miongoni mwa Watanzaia walioshiriki katika mijadala muhimu kuhusu muungano wa Tanganyika na Zanzibar mefariki jana nchini Uingereza alikohamia tangu mwaka 1968.

Katika harakati hizo, alitoa pendekezo la jina ìTanzania,î ambalo lilitokana na mchanganyiko wa majina ya Tanganyika na Zanzibar, na hatimaye likakubaliwa rasmi na viongozi wa wakati huo, akiwemo Mwalimu Julius Nyerere.

Katika mahojiano na waandishi wa habari miaka kadhaa nyumba Mohammed aliwahi kutoa ufafanuzi kuhusiana na jinsi alivyobuni jina hilo loa Tanzania.

Alisema kwa muongozo wa Mungu alichukua herufi tatu za kwanza za Tanganyika (TAN) na herifi tatu za Zanzibar (ZAN) na kisha akaongeza (I) kutoka kwa jina lake Iqbal na Imani yake katika Uislamu. Hatimaye akakumbuka uhusiano wake na madhehebu ya Ahmadiyya na akaongeza (A) ili kuheshimu madhehebu hayo, na hivyo TANZANIA ikatokea.

Mohammed Iqbal alizaliwa katika kipindi cha ukoloni Agosti 8, 1944 na alihusika kwa kiasi kikubwa katika mijadala ya utaifa na harakati za ukombozi wa Tanganyika.

Alikuwa mtu mwenye uelewa wa kina kuhusu historia, utambulisho wa kitaifa, na umuhimu wa mshikamano wa bara na visiwa.

Mnamo mwaka 1964, Tanganyika na Zanzibar ziliungana na kuunda taifa jipya. Kulikuwa na mjadala wa jina gani lingeweza kubeba dhana ya umoja wa nchi hizo mbili, na hapo ndipo Mohammed Iqbal alipoleta wazo la ìTanzaniaîójina lililopokelewa kwa furaha na hatimaye kuwa rasmi.

Katika maisha yake, Iqbal aliendelea kuwa mchangiaji mkubwa katika mijadala ya maendeleo ya kitaifa na umuhimu wa utambulisho wa Tanzania. Kupitia mchango wake, jina ìTanzaniaî limebaki kuwa alama ya mshikamano wa Watanzania na kiashiria cha historia ya taifa.

Kwa kifo cha Mohammed Iqbal, taifa limepoteza mtu muhimu aliyetoa mchango mkubwa katika historia yake. Serikali, viongozi wa kisiasa, wasomi, na wananchi kwa ujumla wanaendelea kuomboleza kifo chake huku wakikumbuka mchango wake usiosahaulika.

Urithi wa Iqbal utaendelea kuishi kupitia jina ìTanzania,î ambalo linawakilisha umoja, mshikamano, na utaifa wa Watanzania wote.

Iqbal amefariki akiwa na miaka 80, na chanzo cha kifo chake kimetokana na kuugua kwa takribani miaka 10, na alikuwa chini ya uangalizi wa karibu nyumbani kwake.

# 20 MBARONI KWA KULA MCHANA MWEZI MTUKUFU WA RAMADHANI

NA MWANDISHI WETU

IKIWA ni siku ya tatu tangu Waislamu duniani wakiwa wameanza mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani Polisi wa Kislamu katika jimbo la Kano, kaskazini mwa Nigeria wamewakamata Waislamu 20 waliokutwa wakila mchana hadharani wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan ambapo pia Watu watano wamekamatwa kwa kuuza chakula huku Naibu kamanda wa Polisi Mujahid Aminudeen akisisitiza kuwa msako huo utaendelea mwezi mzima.

Aminudeen amesema hatua hiyo inalenga kudumisha heshima ya Ramadhan kwani Waislamu wanapaswa kufunga kuanzia alfajiri hadi jua linapozama pia ameeleza kuwa wale waliokamatwa tayari wamefikishwa katika Mahakama ya Sharia kwa ajili ya kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mbali na hilo Polisi wa kiisalmu wa Hisbah pia wamewakamata Watu waliovaa mavazi yanayokiuka maadili ya Kiislamu wakiwemo waliokuwa na nywele zisizoruhusiwa na Madereva wa Bajaji waliowachanganya Abiria wa jinsia tofauti.

Mfumo wa Sharia umeendelea kutumika katika baadhi ya majimbo ya kaskazini mwa Nigeria kwa Waislamu tangu kuanzishwa kwake zaidi ya miaka 20 iliyopita na kutoa adhabu kwa wale wanaokiuka na kukamatwa wakila hakula mwezi mtukufu.



# CCM YAWAWEKA MGUU SAWA WENYEVITI WAKE




NA MWANDISHI WETU

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewataka wenyeviti wa serikali za mitaa waliochaguliwa katika uchaguzi uliofanyika Novemba Mwaka jana kutanguliza huduma na utumishi kwa wananchi wao, kwani waliomba utumishi na wawakiwakilishe chama kama walivyoaminiwa.

Katibu wa Halmashauri Kuu (NEC), Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla ameeleza hayo leo Machi 4, 2025 wakati akizungumza katika mkutano wa viongozi wa chama na jumuiya ngazi ya shina, tawi, kata na wilaya katika Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es salaam, ikiwa ni siku ya kwanza ya ziara yake ya siku tano katika mkoa huo.

Makalla ambaye pia ni mlezi wa Mkoa wa Dar es salaam amepongeza jitihada kubwa zilizofanyika katika uchaguzi wa serikali uliopita na kufanikisha chama hicho kupata ushindi wa mitaa 163 kasoro mmoja ambayo ni sawa na asilimia 99.9 katika mkoa huo.

Aidha, Makalla amesisitiza kuwa wenyeviti hao waliopata kuubeba utumishi vtema na kuwatumikia wananchi na kuwataka kutosimamia na kutotumia mihuri kujipatia fedha kutoka kwa wananchi.

ìNafasi mlizozipata sio za kwenu mmepewa kwa ticket ya chama cha mapinduzi ili mkawatumikie wananchi wenu, mmepata ushindi nendeni mkakiwakilishe Chama Cha Mapinduzi vizuri na kwa ukubwa wake zifanyeni ofisi zenu kuwa kimbilio la wananchi,î amesema Makalla.

Ameongeza: ìMkawe sehemu ya utumishi kwani mliomba utumishi wananchi wanawahamia tangulizeni utumishi na huduma kwa wananchi wenu bebeni utumishi wa kuwatumikia wananchi, nitashangaa mwenyekiti anayesimamia mwananchi alipe muhuri ili apate hudumaî

Akizungumza katika mkutano wa viongozi wa chama na jumuiya ngazi ya shina, tawi, kata na wilaya katika Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es salaam CPA, Makalla amesema kuwa CHADEMA inafanya Makosa kuwahadaa wananchi wasijiandikishe kwa madai kuwa hakutakuwa na uchaguzi.

Amesisitiza kuwa uchaguzi utafanyika kwa mujibu wa sheria na katiba, na kwamba madai ya CHADEMA kwamba ìNo Reform, No Electionî ni propaganda zisizo na msingi na hivyo zipuuzwe.

Vilevile amewataka wenyeviti wa serikali za mitaa waliochaguliwa katika uchaguzi uliofanyika Novemba Mwaka jana kutanguliza huduma na utumishi kwa wananchi wao, kwani waliomba utumishi na wawakiwakilishe chama kama walivyoaminiwa.

# DK. BITEKO: AFRIKA IPO MBELE KWA AJENDA MABADILIKO YA TABIA NCHI

NA MWANDISHI WETU



NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema licha Bara la Afrika kuwa na mchango mdogo katika uchafuzi wa hali ya hewa, nchi za Afrika bado zimekuwa mstari wa mbele katika kuendesha ajenda ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuijumuisha katika mifumo yao ya kisheria na udhibiti ikiwemo ya kuhakikisha kuwa nchi zinahama kutoka kwenye matumizi ya nishati chafu na kutumia nishati safi ili kuiepusha dunia na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Dkt. Biteko amesema hayo jana wakati akifungua Mkutano wa awali kuelekea Kongamano na Maonesho ya Petroli ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCEí25) litakaloanza rasmi kesho ambapo mkutano huo wa awali ulilenga kujadili mipango na mikakati itakayopelekea matumizi ya nishati safi katika maeneo mbalimbali ikiwemo kupikia na vyombo vya usafiri (CNG).

Amesema mkutano wa EAPCEí 25 ni jukwaa muhimu kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wadau wengine kujadili mipango na mikakati kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi hasa ikizingatiwa kwa sasa dunia inapambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na shughuli za binadamu huku tafiti za kisayansi zikionesha kuwa viwango vya utoaji wa hewa ya ukaa vimeongezeka kwa kiasi kikubwa tangu kufanyika kwa Mapinduzi ya Viwanda.

ì Nataka nichukue nafasi hii kuwaomba wote muutumie mkutano huu kujadili masuala ambayo yatatufanya sisi wana Afrika Mashariki, tuweze kuhama kutoka kwenye matumizi ya nishati isiyokuwa safi kwenda kwenye matumizi ya nishati iliyosafi, lazima mtambue kwamba mkutano huu wa awali haujatokea kwa bahati mbaya, kama jamii tunayo kazi ya kufanya ya kutoka kwenye matumizi ya nishati isiyo safi kwenda matumizi ya nishati safi.î Amesisitiza Dkt. Biteko

Ameeleza kuwa, sheria nyingi zinazopitishwa kwa sasa barani Afrika zinahimiza uchumi wa kijani, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na kuwa na maendeleo endelevu ambapo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa upande wake imeandaa Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi ikiwa ni uthibitisho wa dhamira ya kanda hiyo katika kushughulikia tatizo la mabadiliko ya tabia nchi na kuhimiza matumizi ya nishati safi. Ametaja baadhi ya athari za mabadiliko ya tabia nchi kuwa ni pamoja na ukame mkali, mafuriko, kupotea kwa viumbe hai, kupungua kwa vyanzo vya maji safi, kuyeyuka kwa barafu, na ongezeko la magonjwa yanayohusiana na tabianchi kama vile saratani ya ngozi.

Dkt.Biteko ameeleza kuwa suala la mabadiliko ya tabia nchi linatiliwa mkazo pia katika ngazi ya dunia na hii imepelekea kuwepo kwa mikataba mbalimbali ya kimataifa ukiwemo wa Kyoto, Montreal na Paris ambapo nchi zilizoendelea na zinazoendelea zinaandaa na kutekeleza mikakati inayohusiana na tabianchi ikiwemo kujikita katika matumizi ya nishati safi zisizochafua mazingira ikiwemo Gesi Asilia.

Kuhusu upatikanaji umeme amesema Afrika ndiyo Bara linalokabiliwa na upungufu mkubwa wa nishati duniani, ambapo asilimia 75 ya watu wanaokosa nishati duniani wanapatikana barani humo lakini juhudi zinafanyika ili kuwezesha upatikanaji wa nishati na hili lilithibitishwa kupitia Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati uliofanyika Tanzania Januari mwaka huu ambao uliweka mikakati ya kuongeza upatikanaji wa umeme kwa Waafrika milioni 300 ifikapo mwaka 2030 ambayo ni hatua muhimu kuelekea mabadiliko ya kinishati.

Kuhusu Nishati Safi ya Kupikia amesema mabadiliko yanahitajika ili kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi kwani idadi kubwa ya watu barani Afrika bado wanategemea kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia akitolea mfano nchini Tanzania, takriban asilimia 81 ya kaya zinatumia kuni na mkaa kama vyanzo vyao vikuu vya nishati ya kupikia, hali inayosababisha upotevu wa misitu wa takriban hekta 469,420 kila mwaka akitanabaisha kuwa mwelekeo huo wa kutisha unahitaji hatua za haraka na za pamoja ili kuendeleza ajenda ya nishati safi ya kupikia barani kote.

Amesema katika kukabiliana na changamoto hiyo nchini Tanzania, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni kinara wa ajenda nishati safi ya kupikia kitaifa na kimataifa kwa ujumla amechukua hatua madhubuti kwa kutekeleza Mkakati wa Kitaifa Nishati Safi ya Kupikia (2024ñ2034) ambao unalenga kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Aidha amesema kuwa, matumizi ya gesi asilia kama nishati ya kuendeshea vyombo vya usafiri pia ni muhimu katika kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi akieleza kuwa Serikali ya Tanzania inaendelea kuboresha mazingira kwa wawekezaji binafsi kushiriki katika ujenzi wa Vituo vya Gesi Asilia Iliyoshindiliwa (CNG) na kuboresha sera na mifumo ya udhibiti.

Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga kwa upande wake amesema mkutano huo wa awali unaweka msingi wa Kongamano la 11 la Mafuta kwa Nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki litakaloanza kesho Machi 05, 2025.

ìSiku ya leo kutakuwa na mada mbalimbali zitakazozungumzwa, ambazo zitakuwa na majadiliano yatakayoweka msingi kwa ajili ya mkutano mkuu utakaoanza kesho na kufanyika kwa siku tatu, mkutano huu ni muhimu katika kuwaweka wadau pamoja na kujadiliana masuala ya msingi ambayo yatazisaidia Nchi za jumuia ya Afrika Mashariki katika Sekta ya Mafuta na Gesi.î Amesema Kapinga

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amesema kuwa mkutano huo wa Mafuta na Gesi unaenda sambamba na Maonesho ya bidhaa za mafuta na gesi pamoja na kazi mbalimbali zinazofanyika katika sekta miongoni mwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Ameeleza kuwa, Mkutano umelenga kuangalia namna bora ya kuhama kutoka kwenye nishati zinazochafua mazingira kwenda kwenye nishati safi zisizochafua mazingira ikiwa ni kampeni ya dunia ambayo imetokana na malengo ya dunia ya kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2050 hadi 2060 dunia iwe imeweza kuhamia kwenye nishati safi kwa kiasi kikubwa.

Mhandisi Mramba ameeleza kuwa, katika mkutano huo nchi zitapata nafasi ya kuelezea maendeleo waliofanyika katika eneo la mafuta na gesi ambapo Makatibu Wakuu na Mawaziri watazungumza kuhusu mafanikio, mipango na kazi zilizofanyika tangu kufanyika kwa mkutano uliopita wa EAPCE.

Amesema katika mkutano wa EAPCEí25 wataalam, watafiti na wabunifu mbalimbali watazungumzia ugunduzi wa mafuta na gesi, sehemu ambazo vitalu vinanadiwa na kukaribisha uwekezaji kwa nchi za EAC.

# BARABARA LUDEWA KUPUNGUZA GHARAMA YA KUSAFIRISHA MAZAO

NA MWANDISHI WETU



WANANCHI wa kata ya Lumbiji wilayani Kilosa mkoani Morogoro wameishukuru Serikali kupitia TARURA kuwajengea barabara ya Ludewa ñ Lumbiji yenye urefu wa Km 21.6.

Wananchi hao wanaojishughulisha na Kilimo cha mazao ya chakula na biashara wamefurahia ujenzi wa barabara hiyo kwani imerahisisha kusafirisha mazao kwenda sokoni kwa urahisi.

Mwenyekiti wa kijiji cha Kisongwe, Bw. Festo Sekaila amesema kuwa barabara hiyo ilikuwa imeharibika hadi kupelekea kupata hasara ya mazao yao kutokana na gharama ya usafirishaji kuwa juu.

ìGharama ya kusafirisha gunia moja la mazao ilikuwa kati ya shilingi 30,000 ñ 35,000, lakini baada ya barabara kutengenezwa gharama ya kusafirisha gunia moja imeshuka mpaka kati ya shilingi 10,000 ñ 12,000î, amebainisha.

Naye, Laurian Mkuchu ameeleza kuwa barabara hiyo ni chanzo cha mapato yanayotokana na kilimo cha mazao mbalimbali kama vile tangawizi, mihogo, mbaazi, viazi na maharage lakini changamoto kubwa ilikuwa ni namna ya kuyasafirisha mazao yao ambapo barabara hiyo imekuja wakati muafaka kwa wanakijiji wa Kisongwe na kata ya Lumbiji kwa jumla.

Akielezea manufaa waliyoanza kuyapata kutokana na ujenzi wa barabara hiyo, Bw. Mchuku amesema kuwa kwa sasa wao kama wakulima hususani wa zao la tangawizi wanaona kama maajabu kwani bei ya tangawizi imepanda kutoka bei ya kati ya shilingi 400 ñ 500 kwa kilo moja ya tangawizi hadi shilingi 2500 ñ 3000 .

Kwa upande wake Meneja wa TARURA Wilaya ya Kilosa, Mhandisi Juliana Masalo amesema kuwa kata ya Lumbiji ni eneo ambalo lina kilimo kikubwa cha tangawizi na mboga mboga zikiwemo nyanya, nyanya chungu na pilipili lakini barabara hiyo ilikuwa haipitiki kutokana na eneo hilo kuwa na milima na mabonde ya maji yaani ëSwamp areaí.

Ameongeza kuwa barabara hiyo imetekelezwa chini ya mradi wa RISE sehemu ya uondoaji vikwazo katika barabara chini ya mkopo nafuu toka Benki ya Dunia.


# TANGAZA NASI SASA

*Unatamani kukuza biashara yako kutoka hapo ilipo kuwa kubwa na yenye mantiki zaidi?*

- *Unatamani kuongeza kipato, uelewa na upana wa shughuli zako za kila siku?*
- *Je unataka kuwafikia wateja wako ndani na nje ya nchi kwa kiasi kikubwa ili kukuza biashara na huduma yako?*
- *Fahamu kwamba JAMVI LA HABARI na mitandao yake ya kijamii kama Youtube, Instagram, Facebook, Website na Twitter hutembelewa na maelfu ya wasomaji kila siku Duniani kote.*
- *Hivi unafahamu kuwa JAMVILAHABARI kwa sasa ni moja kati ya Media chache zinazo ongoza kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazotokea nchini na Duniani kwa ujumla?*

*TANGAZA SASA NA JAMVI LA HABARI KWA PUNGUZO KUBWA LA BEI UPATE MATOKEO YA HARAKA.*

*Kwa matangazo yote kama vile minada, kupotelewa kwa vyeti vya shule, matangazo ya makampuni, nafasi za kazi, zabuni za kazi, maonyesho, dawa za asili, taasisi za elimu, taasisi za dini na mengine mbalimbali mbali mbali.*

*Ni rahisi sana, wasiliana nasi kupitia Whatsap namba +255659555744 au tupigie katika +255743777778 au +255659555744 GHARAMA ZETU NISAWA NA BUREE JAMVILAHABARI; TUMECHAGUA KUKUHUDUMIA www.jamvilahabari.co.tz*

# FARU WEUPE WAINGIA NCHINI TOKA AFRIKA KUSINI

NA MWANDISHI WETU

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa mara ya kwanza imepokea Faru Weupe 18 kutoka Afrika Kusini kwa lengo la kuimarisha uhifadhi nchini.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano iliyofanyika jana katika Hifadhi ya Ngorongoro, mkoani Arusha, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, amesema kuwa mradi wa kupandikiza faru hao ni hatua muhimu katika juhudi za uhifadhi nchini.

"Mradi huu wa kupandikiza Faru Weupe ndani ya hifadhi ya Ngorongoro ni jitihada za serikali katika kuimarisha uhifadhi wa wanyamapori na unatekelezwa kwa mara ya kwanza kupitia makubaliano kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na kampuni ya AndBeyond," amesema Chana.

Ameeleza kuwa katika makubaliano hayo, kampuni ya AndBeyond imechukua jukumu la kuwezesha upatikanaji na usafirishaji wa faru hao 18 kutoka Afrika Kusini kwa awamu ya kwanza. Awamu ya pili inatarajiwa kuleta faru wengine 18 ili kufikisha jumla ya faru 36, ambapo wengine watawekwa katika maeneo mengine ya uhifadhi nchini.

Chana amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake za dhati za kukuza na kuimarisha sekta ya uhifadhi, ikiwa ni pamoja na mradi huu wa kupandikiza faru weupe.

Aidha, amebainisha kuwa Faru Weupe ni miongoni mwa wanyamapori walioko hatarini kutoweka na hivyo wameorodheshwa katika makundi yanayolindwa chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo Hatarini Kutoweka (CITES).

"Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za kimataifa, hususan za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), kwa kulinda wanyamapori hawa katika mazingira ya asili badala ya kuwafuga kwenye mashamba maalum au bustani," ameongeza Chana.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, mbali na kuimarisha uhifadhi, Faru Weupe pia watatumika katika elimu ya jamii kuhusu usimamizi wa wanyamapori, kuendeleza tafiti za kisayansi na kuboresha mbinu za uhifadhi wa spishi hiyo.

Kwa upande wake, Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Dk. Elirehema Doriye, amesema kuwa kupokelewa kwa faru hao ni uthibitisho wa dhamira ya Tanzania katika kulinda spishi zilizoko hatarini kutoweka.

"Faru hawa watachangia juhudi za kimataifa za uhifadhi, kuongeza fursa za tafiti na kitaalamu, kukuza utalii, na kuinua uchumi wa jamii. NCAA imejipanga kuhakikisha usalama wao," amesema Dk. Doriye.

Naye, Mwakilishi wa Viongozi wa Kimila kutoka Afrika Kusini, iNkosi Zwelinzima Gumedeunywano, amesema kuwa lengo la kutoa faru hao kwa Tanzania ni kusaidia juhudi za uhifadhi na kuongeza uzalishaji wa faru katika Afrika Mashariki.

"Tafiti zinaonyesha kuwa Faru Weupe watastawi na kuzaliana vizuri katika eneo la Ngorongoro," amesema Gumedeunywano, akisisitiza kuwa Afrika Kusini iko tayari kushirikiana na Tanzania katika juhudi za uhifadhi wa spishi hiyo.



# TAHARIRI

## Nida iondoe usumbufu Ugawaji wa vitambulisho

KWA siku za hivi karibuni vituo vya NIDA katika miji na mikoa mbalimbali vimekuwa vikishuhudiwa msongamano mkubwa wa wananchi wanaoshinda hapo kuanzia asubuhi mpaka majira ya jioni, ofisi zinapofungwa.

Wanachofuata katika ofisi hizo ni utekelezaji wa agizo la Mamlaka ya hiyo iliyowataka wananchi wafuatilie vitambulsho vyao, vinginevyo watasitisha matumikzi ya namba.

Kinachoonekana ni kutokuwa na maandalizi ya uhakika kwani idadi kubwa ya wananchi wanapofika katika ofisi hizo, wamekuwa wakikumbana na usumbufu kutoka kwa walinzi na hata mzunguko unaotakiwa kuufuata kabla ya kuelekezwa namna ya kupata kitambulisho.

Sisi tunaona kuwa njia ile ya awali ya kupeleka vitambulisho katika ofisi za Serikali za Mitaa ilikuwa muafakja lakini ilikikosa uratiubu mzuri.

Katika maeneo mengi ya serikali za mitaa tulikuwa tukishuhudia maelekezo ya uwepo wa vitambulisho vya wananchi lakini walipokuwa wakivifuata hata kama maelekezo yanaonyesha vilikuwepo ofisi husika lakini havikuwepo.

Wananchi wengi walijikuta wakitembea kila kata kutafuta vitambulisho vyao bila kupatikana jambo ambalo liliwakatisha tamaa wengi na kukuta vitambulisho vilivyostahili kuwa huku vimepelekwa kule.

Sisi tunadhani njia ya kurudisha zoezi hilo katika ofisi kuu za NIDA ni nzuri, lakini lingeratibiwa vizuri na kuondoa urasimu ili zoezi liende sawia.

Aidha kurudisha maeneo ya aina hiyo kwa namna moja au nyingine itachochea kutokea vitendo vya kuomba rushwa kwa vile wananchi wengi hawapendi kupoteza muda katika jambo wanaloweza kulifanya kwa kutoa rushwa.

Tunadhani itakuwa ni wakati mzuri kwa Mamlaka, kuliangalia tena zoezi hili na kisha kuamua kufanya mawili, au kuboresha ofisi za Serikali za Mitaa na kata au kuweka mazingira mazuri katika ofisi kuu za NIDA.


## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu - 0762 178 678
Idara Ya Matangazo/Masoko - 0743 777 778,
- 0659 555 744
Idara Ya Usambazaji - 0676807684,
- 0787 288 160

Gazeti hili hutolewa na **JAMVI MEDIA GROUP**
S. L. P 78862, Dar es Salaam
**Tel:** +255 676 807684, 255 743 777778
**Email:** jamvinews@gmail.com
www.jamvilahabari.co.tz




*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (katikati) wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Awali wa Kongamano la Mafuta na Gesi la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCE'25), Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, jana.*

## UCHAMBUZI

# Serikali yasisitiza nidhamu miko ya halmashauri

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ametoa onyo kwa wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi endapo itabainika kuwa vikundi hewa katika maeneo yao vilivyonufaika kupitia mikopo ya asilimia 10, watawajibishwa.

Waziri Mchengerwa ametoa onyo hilo jijini Dodoma wakati wa hafla ya utiaji saini mikataba ya utoaji mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulamavu kati ya halmashauri 10 na benki mitatu.

Amewataka Mkuu wa Mkoa , Wilaya na Wakurugenzi wafuatilie kwakuwa hataki kusikia vikundi hewa. "Nawambia wazi kabisa, tumefika hapa kwasababu kuna watumishi wasio waaminifu ambao walitafuna fedha hizi kwa kukopeshana wenyewe na hawakuwa na sifa ya kupokea mikopo hii."amesema Mchengerwa

Aidha Mchengerwa amesisitiza kuwa uadilifu kwenye fedha hizo na kuwataka wafuatilie vikundi vyote na kuvijua na asisikie vikundi hewa.

"Fedha hizi ni za moto wajibu wetu ni kumsaidia Rais fedha hizi zisiende kuchezewa, naelekeza kikundi hewa kitakachobainika eneo lolote viongozi wa eneo hilo mtapaswa kuwajibika, tumieni vyombo mnavyosimamia kwenye mikoa na wilaya kuhakikisha hakuna vikundi hewa, fedha zisimamiwe na kurejeshwa."amesisitiza

Hata hivyo amesema vikundi vyote vinavyopokea mikopo hiyo vinatakiwa kufanya shughuli za uzalishaji na kurejesha fedha kulingana na mipango ya marejesho.

"Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi tumekubaliana jukumu la usimamizi wa fedha hizi ni la kila mmoja wet una wakati tunamshauri Rais sisi Wizara tulimhakikishia kuanzia kwangu kwamba iwapo kutakuwa na kulegalega kukote mimi na wasaidizi wangu tutalazimika kuwajibika."

Amesema Benki ya NMB itafanya kazi kwenye halmashauri za wilaya za Bumbuli, Itilima, Newala, Manispaa ya Songea, Jiji la Dodoma huku benki ya CRDB itafanya kazi Wilaya za Nkasi, Mji wa Mbulu, Manispaa ya Kigoma na Jiji la Dar es salaam.

Hata hivyo, amesema Benki ya Biashara ya Uchumi itafanya kazi Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

"Zaidi ya Sh.Bilioni 234 zinakusudiwa kupelekwa kwa wananchi kwa njia mbili za utoaji mikopo hiyo ambazo ni kupitia Benki kwa Halmashauri 10 na mikopo iliyoboreshwa kwenye Halmashauri 174.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Tamisemi, Profesa Adolf Ndunguru amesema kuwa kusainiwa mikataba hiyo ni mwanzo wa mapinduzi ya kuhakikisha mikopo hiyo ya asilimia 10 inakuwa na tija tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

# Umuhimu wa mawasilian

NA MWANDISHI WETU



MAWASILIANO ni nyenzo muhimu kwa nchi yoyote ile duniani.

Kwa nchi yenye watu wenye kipato cha kati na maskini kama Tanzania mawasiliano huwa muhimu zaidi katika kukuza uchumi.

Hii ni kwa sababu mawasiliano ni muhimu zaidi katika kuiwezesha familia, kaya, mtaa, kitongoji, kijiji hadi taifa kukuza uchumi kupitia shughuli mbalimbali ambazo pengine bila mawasiliano isingewezekana kuzitekeleza kwa namna yoyote.

Kwa mujibu wa wataalamu, mawasiliano hurahisisha biashara, mazingira ya uwekezaji na usambazaji wa taarifa na hivyo kuruhusu Kampuni, watu binafsi na sekta mbalimbali kufanya kazi kwa urahisi na ufanisi.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni jijini Mwanza na Mkurugenzi wa Masuala ya Kisekta kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mwesiga Felician, alipozungumza kwenye semina ya wahariri, wandishi wa habari na watangazaji wa vyombo vya habari mkoani Mwanza.

Anasema mawasiliano huimarisha umoja, amani na mshikamano wa taifa kwa kuwezesha watu kuelewana na kushirikiana na kupitia mawasiliano, jamii zinaweza kushughulikia changamoto zao kwa pamoja, kueneza ujumbe wa amani na kuepuka migogoro pia.

Anaongeza kwamba viongozi wa serikali na wadau wengine wanaweza pia kutumia mawasiliano kufikia wananchi ili kujenga umoja wa kitaifa na kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kimataifa.

Aidha, anasema mataifa yanatumia mawasiliano rasmi kama ya kidiplomasia na mikutano ya kimataifa kubadilishana mawazo, teknolojia na rasilimali hali inayo ongeza maelewano baina ya mataifa, kuimarisha biashara kimataifa na kuweka maendeleo ya pamoja.

Felician anasema mawasiliano ni mhimili wa maendeleo ya kijamii, kiuchumi, na kisiasa na bila mawasiliano madhubuti, taifa haliwezi kufanikisha maendeleo endelevu na uhusiano imara wa kimataifa.

Kwa kuzingatia umuhimu huo, Felician anasema serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ifanye mapinduzi makubwa ya kupigiwa mfano katika sekta ya mawasiliano kutokana na kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta hiyo.

Takwimu za Sekta

Felician anasema Tanzania imepata mafanikio makubwa kwenye sekta ya mawasiliano na kwamba kwa mujibu wa Ripoti ya Sekta ya Mawasiliano ya robo ya pili ya mwaka wa fedha 2024/2025 inayoishia Desemba 2024, jumla ya laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka milioni 80.7 katika robo ya mwaka i yoishia Septemba, 20 hadi milioni 86.8 kw robo ya mwaka ina oishia Disemba 2024 ik wa ni sawa na ongezek la asilimia 7.7.

Akielezea mchanga uo ya idadi za laini simu za mkononi (P2 na mezani, anasen laini za simu za mko oni na mezani zilizosajiliw kwa ajili ya mawas liano ya binadam

# no katika maisha ya jamii



Endapo wananchi watatoa taarifaa polisi mamlaka husika itafanya jitihada za kawasaka matapeli wanaofanya utapeli kupitia simu.

zimeongezeka kwa takribani milioni 7.8 katika robo mwaka inayoishia Desemba 2024.

Laini za simu kimkoa

Alisema idadi ya laini za simu kwa kila mkoa inaonesha kuwa katika robo ya pili ya mwaka 2024/2025, mkoa wa Dar es Salaam ulishika nafasi ya kwanza kwa kuwa na laini milioni 15.98, ukifuatiwa na mkoa wa Mwanza laini milioni 5.75, Arusha laini milioni 5.23, Mbeya laini milioni 4.99 na Dodoma ilishika nafasi ya tano kwa kuwa na laini milioni 4.64 Feliciana anasema kwenye matumizi ya matumizi ya intaneti asilimia 91 ya Watanzania wamefikiwa na huduma ya kasi ya intanenti ya 3G na asilimia 88 (4G) huku asilimia 20 wakiwa wamefikiwa na matumizi ya 5G.

Anaeleza kuwa kwa sasa watu milioni 23 wanamiliki simu janja. Anasema takribani dakika bilioni 42.5 zilitumika katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2024 ikilinganishwa na dakika bilioni 41.1 katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2024.

Anasema katika kipindi hicho, idadi ya dakika nje ya mtandao ilikuwa kubwa zaidi ikilinganishwa na ndani ya mtandao katika robo ya mwaka iliyoishia Desemba 2024. ìSekta ya mawasiliano ni sekta wezeshi kwa sekta zingine za kiuchumi,î anasema na kuwataka wanahabari kuhakikisha wanaandika kwa kina kuhusu umuhimu na faida za sekta za mawasiliano katika kukuza uchumi wa nchi.

Meneja wa TCRA kanda ya ziwa Mhandisi Imelda Banali anasema lengo la TCRA kutoa semina hiyo kwa waandishi wa habari ni kuwajengea uwezo wa namna ya kuandika na kuchambua repoti na takwimu mbalimbali zinatolewa na

mamlaka ili waiwezeshe jamii kuwa na uelewa mpana wa shughuli zinazofanywa na TCRA.

ìNia yetu hasa ni kupata wandishi wabobezi kutoka mikoa ya kanda ya ziwa watakaokuwa wabobezi wenye weledi na uelewa katika kuandika habari za sekta ya mawasiliano,î anasema. Anasema vyombo vya habari vina nafasi kubwa sana ya kuelimisha jamii kuhusu umuhimu na faida za sekta ya mawasiliano nchini katika kukuza uchumi.

ìTumieni vyombo vyenu na nafasi zenu katika kupeleka elimu hii kwa watu, ili waweze kuifahamu vizuri sekta ya mawasiliano, iweze kuwanufaisha kiuchumi,î anasema.

Hii ni hatua nyingine kwa serikali kuimarisha sekta ya Mawasiliano, ambapo pia tumeshuhudia elimu ikitolewa jinsi ya wananchi kuitumia Teknolojia hii kwa uangalifu hususan kuepuka madhila yakiwemo ya matapeli wa mitandao.

Hivi karibuni Wasiri wa Mawasiliano na Teknolojia ya habari, Jerry Silaa amewataka wananchi wanaotapelewa kwa njia ya mitandao ya simu kutoa taarifaa katika mamlaka husika ili hatua kali zaidi zichukuliwe ili kukomesha utapeli huo

Alitoa rai hiyo jijini Arusha katika mkutano maalumu na waandishi wa habari kuhusu kampeni kabambe ya "SITAPELIKI "inayolenga kutoa elimu kwa jamii

Waziri Silaa anasema wananchi wanaotapeliwa watoe taarifaa zao kwa Jeshi la polisi lakini pia kwa Mamlaka ya mawasiliano Tanzania (TCRA)

"Endapo wananchi watatoa taarifaa polisi mamlaka husika itafanya jitihada za kawasaka matapeli wanaofanya utapeli kupitia simu

Pia amesisitiza kwa wadau wote wa vyombo vya habari kushiriki katika utoaji wa elimu kwa jamii juu ya kampeni ya "SITAPELIKI" ambayo ni kampeni endelevu itakayokwenda kudhibiti vitendo vya utapeli na ulaghai kupitia mitandao.



# NLD YAIFUATA CCM KUSHIRIKI UCHAGUZI MKUU




NA MWANDISHI WETU

CHAMA cha National League for Democrats (NLD), kimetangaza kuanza kwa mchakato wa ndani ya chama wa kuwapata wagombea wa nafasi za Udiwani, Ubunge na Rais kuelekea Uchaguzi Mkuu, utakaofanyika mwezi Oktoba mwaka huu.

Aidha chama hicho kimetangaza neema kwa wagombea wanawake, kuwa hawatotoa ada yoyote wakati wa kuchukua fomu, lengo ni kuwapa fursa ya kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi.

Akizungumza mapema leo na waandishi wa Habari, Katibu mkuu wa NLD Taifa ,Doyo Hassan Doyo, amesema, chama hicho kimelenga kusimamisha wagombea katika majimbo yote ya Uchaguzi kuanzia Udiwani, Ubunge pamoja na nafasi ya Rais,

"Chama chetu kitashiriki Uchaguzi Mkuu, hivyo kwakutambua hilo, leo tunatangaza rasmi kuwa ,chama kimefungua milango ya kuanza mchakato wa kuwapata wagombea wa nafasi za Udiwani, Ubunge na Rais, hivyo watu wote wenye sifa wanakaribishwa kushiriki, ili ukidhi sifa ya kushiriki mchakato huu ni lazima uwe Mwanachama hai wa Chama chetu," aliongeza Doyo Doyo alisema kuwa, kwaupande wa wagombea Wanawake hawatolipa ada yoyote wakati wa mchakato wa kuchukua fomu,

"Chama chetu, kwa mapenzi mema kabisa, na kwakuona umuhimu wa akinamama, tumeamua kuwa, wanawake wote watakaojitokeza kugombea nafasi za uongozi ndani ya chama chetu, hawatolipa ada yoyote ya fomu, hii itasaidia kuongeza hamasa na kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi za Udiwani, Ubunge na Rais"Alisisitiza Doyo

Aliongeza kuwa katika kikao cha Kamati Kuu ya Chama hicho Februari 23, mwaka huu, chama hicho kilianzimia kuwa kabla ya Uchaguzi Mkuu ni lazima kufanyike mikutano ya hadhara na ndani ili kupata wagombea wenye uwezo pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi 'INEC' nilazima iweke wasimamizi wa Uchaguzi wenye weledi, ili uchaguzi uwe huru na haki.

Hicho ni chama cha pili cha siasa kilichotangaza kushiriki uchaguzi Mkuu kabla ya hapo CCM ambacho ni chama tawala nacho kilithibitisha kushiriki tukio hilo la kikatiba.

Hivi karibuni Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Mgombea Mwenza wa Urais Tanzania Bara, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, amewahimiza wanachama wa Jumuiya ya Umoja wa Wazazi kuendelea kujipanga vyema ili kuhakikisha chama kinashinda Uchaguzi nafasi za Ubunge na Udiwani kwa kuzingatia sera na maadili.

Ilikuwa ni katika kikao cha Kamati ya Utekelezaji ya Jumuiya hiyo jijini Dodoma, Dkt. Nchimbi alisisitiza kuwa CCM ni chama kinachojikita katika sera na maendeleo, si katika matusi au kejeli.

"Chama chetu kimefanya mambo makubwa kwa maendeleo ya taifa. Tunapaswa kuendelea kusimamia hoja zenye mashiko na si kutumia lugha zisizofaa. Tunapaswa kuwa mfano wa kuheshimu watu na kuzungumzia maendeleo yanayoonekana," alisema.

Aidha, alieleza kuwa serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanikisha mambo mengi ambayo yanaweza kuwahamasisha wananchi kuendelea kukiamini chama.

"Tunayo mengi ya kuwaambia Watanzania kuhusu maendeleo yaliyofikiwa, hatuna sababu ya kutumia lugha za kejeli. Hayo tuwaachie wale wasiokuwa na hoja za msingi," aliongeza.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wazazi Taifa, Fadhili Maganya, alisema kuwa ujio wa Dkt. Nchimbi katika kikao hicho ni ishara ya heshima kwao.

"Uwepo wako hapa umetupa faraja kubwa. Tumekukaribisha ili usikilize mawazo yetu na kutushauri. Hii ni historia, kwani sisi ndiyo jumuiya ya kwanza kuketi na wewe tangu uteuliwe kuwa mgombea mwenza," alisema Maganya.

Kikao hicho kilitoa fursa kwa viongozi wa Umoja wa Wazazi kujadili masuala muhimu yanayohusu ustawi wa jumuiya na mchango wake katika mustakabali wa chama kuelekea uchaguzi ujao.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi aliyasema haya kwenye Kikao cha Kamati ya Utekelezaji ya Baraza Kuu la Umoja wa Wazazi, Jumuiya ya CCM, ambacho alialikwa na kushiriki akiwa mgeni maalum, leo Jumamosi tarehe 8 Februari 2025, katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

"Katika kikao chetu cha hivi karibuni, chama chetu kiliazimia kuwa ni lazima tufanye mikutano ya hadhara kwakipindi hiki ili tupate wagombea wenye uwezo, lakini pia kwa upande wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi 'INEC' ni lazima iweke wasimamizi wa Uchaguzi wenye weledi ili Uchaguzi uwe huru na haki, na usiwe na dosari," alisisitiza Doyo

# CMSA YABAINISHA MAFANIKIO YAKE

NA MWANDISHI WETU

MAMLAKA ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) imesema katika mwaka 2024 kumekuwa na mafanikio makubwa ambayo yamewezesha pia thamani ya uwekezaji katika masoko ya mitaji kuongezeka kwa asilimia 24.7 na kufikia Sh.trilioni 46.7 katika kipindi kilichoishia Desemba 2024, ikilinganishwa na Sh.trilioni 37.4 katika kipindi kilichoishia Desemba 2023.

Pia thamani ya uwekezaji katika hisa za kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa yaani imeongezeka kwa asilimia 22.3 na kufikia Sh.trilioni 17.87 katika kipindi kilichoishia Desemba 2024, ikilinganishwa na Sh.trilioni 14.61 katika kipindi kilichoishia Desemba 2023.

Aidha, thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja imeongezeka kwa asilimia 41.6 na kufikia shilingi trilioni 2.6 katika kipindi kilichoishia Desemba 2024,ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.8 katika kipindi kilichoishia Desemba 2023.

Mafanikio hayo yameelezwa leo Februari 26,2025 jijini Dar es Salaam na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana(CMSA), CPA. Nicodemus Mkama wakati akitoa tathimini yq utendaji wa masoko ya mitaji kwa mwaka 2024.

ìCMSA ina jukumu la kuendeleza na kusimamia masoko ya mitaji hapa nchini, ikiwa ni pamoja na kuwezesha utoaji wa bidhaa mpya na bunifu zinazovutia wawekezaji wa ndani na kimataifa. Katika kutekeleza jukumu hili, katika kipindi cha mwaka 2024, masoko ya mitaji yamepata mafanikio.î

Ametaja baadhi ya mafanikio mengine ambayo yamepatikana ni uwepo wa Bidhaa Mpya na Bunifu ambapo amesema mwaka 2024 umeshuhudia utoaji wa bidhaa mpya na bunifu zinazovutia wawekezaji wa ndani na wa kimataifa.

Amefafanua mathalani, Hatifungani ya kijani ya taasisi ya umma iliyotolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Jiji la Tanga (Tanga-UWASA) kwa ajili ya kutekeleza miradi ya miundombinu ya maji na utunzaji wa mazingira, ambayo ilikusanya Sh.bilioni 54.72, na kuvuka lengo la kukusanya shilingi bilioni 53.2, sawa na mafanikio ya asilimia 103

Vilevile, Hati Fungani ya Miundombinu ya Samia iliyotolewa na Benki ya CRDB ilikusanya Sh.bilioni323.09, kuvuka lengo la kukusanya shilingi bilioni 150,sawa na mafanikio ya asilimia 215.4.

Amesema fedha zilizopatikana zinatarajiwa kuwezesha wakandarasi wa ndani wanaofanya kazi na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA), kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara vijijini na mijini.

Aidha, Hatifungani kwa ajili ya kuendeleza kampuni ndogo na za kati za ujasiriamali (SMEs) iliyotolewa na Benki ya Azania, ambapo kiasi cha Sh.bilioni 63.3kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 210.9.

Pia, Hatifungani aina ya Sukuk iliyotolewa na kampuni ya iTrust Finance, kwa ajili ya kuwekeza katika biashara ndogo na za kati zinazokidhi misingi ya Shariah, ambapo kiasi cha Sh.bilioni 13.27 kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 265. Vile vile, Mauzo ya Hisa Stahiki za Benki ya DCB zenye thamani ya shilingi bilioni 10.74, ambapo mauzo haya yamepata mafanikio ya asilimia 100.

CPA.Mkama pia amesema mwaka 2024, umeshuhudia mwamko mkubwa wa utoaji bidhaa mpya na bunifu katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja, hivyo kuweka wigo mpana wa fursa za uwekezaji kwa watanzania wa kada mbalimbali, ikiwa ni Pamoja na vijana, wanawake na makundi maalumu.

ìCMSA iliidhinisha Mifuko ya Uwekezaji inayoendeshwa na Kampuni ya iTrust Finance Limited, ambapo mifuko mipya mitano ilizinduliwaóiSave, iCash, Imaan, iIncome, na iGrowth.

ìVilevile, Zan Securities na Orbit Securities walizindua mifuko ya Timiza na Inuka, huku Alpha Capital ikianzisha Mfuko wa Halal. Aidha, Sanlam Investments East Africa ilizindua SUTS - SANLAM Unit Trust Scheme, ikijumuisha Sanlam Pesa Money Market Fund na US Dollar Fixed Income Fund.

ìKutokana na juhudi hizi, thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (NAV) iliongezeka kwa asilimia 41.63, kutoka shilingi trilioni 1.84 mwaka 2023 hadi shilingi trilioni 2.61 mwaka 2024. Ukuaji huu umetokana na mikakati ya utoaji wa elimu kwa umma unaofanywa na wadau katika masoko ya mitaji na matumizi ya mifumo ya kidijitali, ambayo imerahisisha upatikanaji wa huduma za masoko ya mitaji mijini na vijijini.îAmesema.

Kuhusu matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano amesema imekuwa na mchango mkubwa katika kuongeza mauzo katika soko la hisa. Matumizi ya teknolojia ya Habari, ikiwa ni pamoja na matumizi ya simu za mkononi yameongeza ushiriki wa wawekezaji wa ndani, hivyo kuongeza ukwasi katika soko la hisa.

Amefafanua katika mwaka 2024, asilimia 24.33 ya mauzo ya hisa yametokana na matumizi ya teknolojia ya habari, ikilinganishwa na asilimia 4.84 mwaka 2023 huku akitoa rai kwa wadau katika masoko ya mitaji kushirikiana na CMSA katika mwaka wa Fedha 2025/2026 kutekeleza mikakati mbalimbali.

Ametaja baadhi ya mikakati hiyo kuongeza juhudi za kutekeleza Mpango Mkakati wa elimu kwa umma kuhusu fursa na faida zinazopatikana kwenye masoko ya mitaji, ikiwa ni pamoja na kutoa machapisho mbalimbali magazetini.

Pia kushiriki kwenye mahojiano ya vipindi vya Redio na Runinga, kutoa semina, warsha na makongamano kwa makundi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na vijana, wanawake na walemavu. Hafla ya leo iliyoandaliwa na Vertex International Securities ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati huo.

Mengine ni kuongeza idadi ya bidhaa, ambapo Mamlaka itaendelea kutoa miongozo ya utoaji na usimamizi wa bidhaa na huduma mpya, bunifu, na zenye mlengo maalum.

Pia Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kutoa huduma za masoko ya mitaji, ambapo CMSA itapitia na kuidhinisha mifumo ya kidigitali inayowezesha ushiriki mkubwa wa wananchi kwenye masoko ya mitaji.

ìHatua hii inatarajiwa kuongeza ushiriki wa wananchi mijini, vijijini katika masoko ya mitaji, na hivyo kuchangia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Tatu wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha.Kwa ujumla, katika kipindi cha mwaka 2024, masoko ya mitaji nchini Tanzania yameimarika na kuonyesha ukuaji mzuri na wa kuridhishaÖ

ìYakichochewa na utoaji wa bidhaa mpya na bunifu, matumizi ya teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Utoaji elimu kwa umma ulioleta mwamko mkubwa kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa. Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) itaendelea kutekeleza mikakati yenye lengo la kuchagiza na kujenga uchumi shindani kwa maendeleo ya watu,îamesema CPA.Mkama.



# MAVUNO YA KAHAWA YATIKISA MKOANI RUVUMA

NA MWANDISHI WETU

WAKULIMA wa zao la kahawa wanaohudumiwa na Chama cha Msingi cha Ushirika KImuli Amcos kata ya Utiri Wilaya ya Mbinga Mkoani Ruvuma, wamefanikiwa kuzalisha tani 105,986.95 za kahawa zilizowaingizia zaidi ya Sh.bilioni 14,022,174,698.40 kuanzia Msimu wa kilimo 2021/2022 hadi 2024/2025.

Katibu wa Chama hicho Aron Komba amesema, katika msimu 2021/2022 wakulima walizalisha tani 548,551 zenye thamani ya Sh.bilioni 3,299,453,120,msimu wa kilimo 2022-2023 walizalisha tani 455,643 ambazo ziliwaingizia Sh.bilioni 3,065,405,776.40.

Aidha alisema, msimu wa 2023/2024 Wakulima ambao ni Wanachama wa Kimuli Amcos walizalisha jumla ya kilo 585,288 zenye thamani ya Sh.bilioni 2,929,893,908 na msimu 2024/2025 walizalisha kilo 530,253 ambazo waliuza Sh.bilioni 4,727,421,894 kupitia njia ya minada.

ìPia kwa muda wa miaka minne ya Uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, tumetoa mikopo ya pembejeo yenye thamani ya Sh.bilioni 3,056,783,867 kwa Wakulima 7,005 wanaojishughulisha na kilimo cha kahawa na mazao mengine ya chakula na biasharaîalisema Komba.

Kwa mujibu wa Komba, msimu wa kilimo 2022/2023 wametoa mikopo ya pembejeo ya Sh.957,343,812 kwa wanachama 2,137 mwaka 2023/2024 Sh.917,834,200 kwa Wanachama 2,381 na mwaka 2024/2025 wametoa mikopo yenye thamani ya Sh.1,181,605,855 iliyokwenda kwa Wananchama 2,487.

Alisema, mikopo hiyo imewasaidia Wanachama kulima kwa tija na kuongeza uzalishaji kwani hapo awali walikuwa wanaangaika kutafuta pembejeo ambazo ziliuzwa kwa bei kubwa kati ya Sh.165,000 hadi 170,000 kwa mfuko mmoja wa kilo 25.

Alisema, hali hiyo ilipelekea baadhi ya wakulima kukata tamaa na kutoendelea na shughuli zao za kilimo kutokana na kushindwa kumudu gharama ya pembejeo ambapo, amempongeza Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, kwa kuanza utaratibu wa kutoa pembejeo za ruzuku kwa zao la kahawa.

Komba, ameiomba Serikali kuendelea kutoa pembejeo za ruzuku kwa zao la kahawa ili kuwapunguzia wakulima mzigo mkubwa wa kununua pembejeo kwa bei ya juu na kuongeza upatikanaji wa pembejeo za ruzuku ili wakulima waweze kuzalisha kwa wingi.

ìNaishauri Serikali kama inataka kufanikisha mpango wake wa kutouza kahawa ghafi basi ituwezeshe kwa kutujengea miundombinu ili tuweze kukaanga kahawa tunayozalisha kwa ajili ya matumizi ya sisi wenyewe na watu wengine na nyingine tuuze kwenye soko la nje"alise ma Komba.

***Ametoa ombi kwa Serikali kupitia Wakala wa Barabara za mijini na vijijini(Tarura) Wilaya ya Mbinga, kukamilisha ujenzi wa Barabara ya lami ya Utiri-Mahende kwa kiwango cha lami ili iweze kusaidia wakulima kusafirisha mazao kupeleka sokoni kwa haraka kwani barabara hiyo inapita kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa kahawa.***



Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Amcos ya Kimuli Yordan Komba alisema, katika kipindi cha miaka minne Chama hicho kimepiga hatua kubwa kwa kuongeza Wanachama kutoka 364 tangu kilipoanzishwa mwaka 1993 hadi 1,700 mwaka 2024.

Aidha, ameiomba Serikali kupitia maafisa Ugani kwenda kwa wakulima kuwapa utaalam na mbinu za kilimo cha kisasa zitakazo wasaidia kuongeze uzalishaji na kupata mavuno mengi.

Mkulima na Mwanachama wa Chama hicho Gisat Komba alisema, kwa muda wa miaka minne uzalishaji wa kahawa umeongezeka na hali hiyo imetokana na upatikanaji wa pembejeo za ruzuku zinazotolewa na Serikali ambazo zimehamasisha watu wengi hasa vijana kujikita kwenye kilimo cha zao hilo.

Hata hivyo alisema, changamoto kubwa ni soko la uhakika kwani wanunuzi wana tabia ya kujipangia bei ya kahawa bila kuwashirikisha wakulima jambo linalowaumiza sana kwa sababu wanatumia gharama kubwa katika uzalishaji wake.

Kwa upande wake Afisa Mtendaji wa kata ya Utiri Libaba Gervas Libaba alisema, kata hiyo ni maarufu kwa kilimo cha zao la kahawa na Wananchi wanajitahidi sana kulima, lakini changamoto iliyopo ni upatikanaji wa pembejeo za ruzuku.

Ametoa ombi kwa Serikali kupitia Wakala wa Barabara za mijini na vijijini(Tarura) Wilaya ya Mbinga, kukamilisha ujenzi wa Barabara ya lami ya Utiri-Mahende kwa kiwango cha lami ili iweze kusaidia wakulima kusafirisha mazao kupeleka sokoni kwa haraka kwani barabara hiyo inapita kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa kahawa.

Baadhi ya Wakulima wa zao la Kahawa wa kijiji cha Utiri Wilaya ya Mbinga Mkoani Ruvuma wakiangalia uzalisha kwenye miche ya kahawa katika moja ya shamba linalomilikiwa na Chama cha Msingi cha Ushirika Kimuli Amcos.



# MSAADA WAKISHERIA WA DK SAMIA WAPONGEZWA




NA MWANDISHI WETU

MKUU wa Wilaya ya Longido, Salum Kalli amesifu juhudi za wizara ya Katiba na Sheria kwa kuwaletea wananchi huduma ya msaada wa kisheria bure na kusisitiza kuwa wananchi wa Arusha wanapaswa kuitumia ipasavyo kwa manufaa yao na jamii kwa ujumla.

Pia amewataka wakazi wa mkoa wa Arusha kuchangamkia fursa ya kipekee ya kupata msaada wa kisheria kupitia Mama Samia Legal Aid Campaign inayoendelea jijini Arusha.

Akizungumza Juzi, alipotembelea mabanda ya huduma za kisheria katika viwanja vya TBA jijini Arusha, Kalli amesema kuwa kampeni hiyo itadumu kuanzia Machi 1 hadi Machi 8, 2025 na ni nafasi muhimu kwa kila mwananchi mwenye changamoto za kisheria kufika na kupata msaada bure.

ìHii ni fursa adhimu kwa kila mwenye changamoto za kisheria. Kuanzia masuala ya mirathi, migogoro ya ardhi, ndoa, na mengineyo. Napenda kuwaalika wananchi wote, hususan wanawake wanaokabiliwa na changamoto hizi, kufika na kupata msaada wa kisheria bila malipo,î amesema Kalli.

Aidha, ametoa mfano wa mama mjane ambaye amenyangíanywa mali alizochuma na mume wake baada ya kufariki. Kupitia kampeni hii, mama huyo na wengine wenye changamoto kama hizo wanaweza kupata haki zao kwa msaada wa wataalam wa sheria waliopo kwenye mabanda hayo.

ìHii ni kampeni muhimu inayohakikisha haki inapatikana kwa wote, hususan wale waliokosa sauti ya kutetea haki zao,î ameongeza.

Mama Samia Legal Aid Campaign inaendelea jijini Arusha hadi Machi 8, 2025, ikiwa na lengo la kuwasaidia wananchi kupata haki zao bila gharama yoyote.

Wakati msaada huo ukiendelea kupokewa kwa matumaini sehemu mbalimbali nchini hivi karibuni Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini, amewataka wananchi kutoa maelezo sahihi kwa watoa huduma za msaada wa kisheria ili kufanikisha kutatua changamoto zinazowakumba, na kuhakikisha kuwa migogoro ya ardhi, mirathi, ndoa na masuala mengine ya kisheria yanapata ufumbuzi kwa wakati.

Sagini ameyasema hayo leo mkoani Arusha wakati alipotembelea banda la Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na mabanda mengine kuelekea wiki ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambayo itafanyika Machi 8 mwaka huu mkoani Arusha.

Aidha maadhimisho hayo ambayo yanatanguliwa na maonyesho kutoka kwa taasisi na mashirika mbalimbali, amewataka wananchi kutumia fursa hiyo kufika kwa wingi katika mabanda hayo kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali za kisheria sambamba na kutatuliwa kero za zinazowakabili kwa wakati.

Aidha Sagini amekazia umuhimu wa kampeni ya Mama Samia Legal Aid inayolenga kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi wenye changamoto za kisheria.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda ameagiza watoa huduma za msaada wa kisheria kwenye kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa kisheria ya Mama Samia, kuhakikisha kuwa wananchi wote waliofika kupata msaada wa kisheria wanasikilizwa na kutatuliwa changamoto zao kikamilifu.

Makonda amesema kuwa ,lengo la wananchi kufika kwenye mabanda hayo ni ili kupata haki zao za msingi kwa wakati na kutatuliwa kero zao kupitia kampeni ya Samia Legal Aid inayotolewa viwanja vya TBA.

Makonda amesema wananchi wanaofika katika banda hilo wanatakiwa kusikilizwa na kuhudumiwa ili waweze kutoa malalamiko yao ikiwemo kuangalia kwa makini changamoto zao hususani katika idara ya kazi, sheria, haki za watoto na mengineyo.

Aidha Makonda ametumia fursa hiyo pia kuwasihi wananchi wa mkoa wa Arusha kujitokeza kwa wingi kupatiwa msaada huo wa kisheria ili migogoro yao iweze kutatuliwa kupitia uwezeshaji uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan uliotokana na wazo lake hili la kuwa na kampeni ya kitaifa ili kuwafikia wananchi wanyonge na wale wanaokosa haki zao kulingana na sheria.

Nao baadhi ya wananchi waliofika kupata huduma kwenye banda hilo wamesema kuwa, wanashukuru serikali kwa kuwasogezea huduma karibu ili waweze kutatuliwa changamoto zao na kuweza kupata elimu zaidi kuhusu maswala ya kisheria ambayo yamekuwa ni changamoto kwa wengi wao kutokana na kutozijua sheria mbalimbali .

ìKwa kweli tunashukuru sana kwa jambo hili kwani limetupa fursa kubwa sisi kuweza kujifunza na hata kutatuliwa changamoto zetu ambazo zilikuwa zimedumu kwa muda mrefu na kuweza kupata huduma hiyo bure pia tunamshukuru sana Rais Samia kwa kuanzisha hii kampeni ambayo inalenga kutatua changamoto mbalimbali za mambo ya kisheria.îamesema.

# Michezo Kimataifa

## Tetesi za soka



CHELSEA wanaamini wanaweza kufanya dili kwa ajili ya mlinzi wa Sporting Ousmane Diomande msimu wa joto - chini ya kipengele cha ukubwa wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 21. (TeamTalk),



JUVENTUS wameipa Chelsea ruksa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal, hii imetokana na mazungumzo mazuri kati ya klabu hizo na pia maslahi yaliyoridhiwa na pande hizi mbili.




1

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Vinicius Jr, atakuwa na fursa ya kuhamia ligi kuu ya Saudi Arabia kwa pauni milioni 200 msimu wa joto, wakati atakapokuwa imesalia miaka miwili kwenye mkataba wake na Real Madrid. (Telegraph)

BAADA ya kulaulimiwa kwa muda mrefu kuwa tatizo la Arsenal ni kudharau kufaya usajili hasa eneo la ufungaji, hatimaye klabu hiyo imesikia kilio hicho na sasa imeanza mawindo makali ili kutibu pengo lililopo, kufutia mkakati huyo klabu hiyo imeingia chimbo na kumnasa Straika makali Raia Slovenia anayekipiga katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani





## TFF YABARIKI ULIPAJI KODI NCHINI

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania-TFF, Bw. Wallace Karia, amekubali mapendekezo ya Serikali na kuahidi kuwa suala la ulipaji kodi ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa. Aidha ameahidi kuwa watalichukulia kwa uzito suala la Kodi katika michezo yote ya mpira wa miguu inayosimamia na Taasisi hiyo.

Kauli hiyo imetolewa katika kikao cha majadiliano kati yake na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Na (Mb) na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Profesa Palamagamba Kabudi. Kikao hicho pamoja na masuala ya kodi walijadili maendeleo na changamoto zinazoikabili sekta ya michezo hususan mpira wa miguu nchini. Katika mazungumzo hayo yaliyofanyika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam, Serikali imeipongeza TFF na Bodi yake ya Ligi, kwa kusimamia kwa weledi masuala ya maendeleo ya soka na kuliletea Taifa heshima kubwa barani Afrika kiasi cha kupewa jukumu la kuandaa mashindano ya CHAN na AFCON. Pia serikali ilikubaliana na namna tasnia ya utamaduni, sanaa na michezo inavyoweza kutumika kuhamasisha uzalendo wa kulipa kodi kwa hiari, kupitia kampeni ya kudai na kutoa risiti kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Majadiliano hayo yaliwashirikisha viongozi wa juu wa Wizara ya Fedha, akiwemo Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya, Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA, Bw.Yusuph Mwenda, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania- TFF, Bw. Wallace Karia, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Bw.. Almas Kasongo, viongozi waandamizi wa Wizara ya Fedha, pamoja na Taasisi zinazosimamia michezo nchini.



# SIKIA KISA CHA TALAKA INAYOSISIMUA - 1

NA MWANDISHI WETU

MAHUSIANO ya kimapenzi ya Mfalme wa jamii ya Wazulu kutoka Afrika Kusini yamezua mjadala nchini humo, huku gumzo linalohusiana na maisha yake ya kibinafsi likisambaa kwa kasi kama moto wa nyikani katika jamii hiyo ambayo inakumatia utamaduni wake. Mfalme wa Zulu anasemakana kuvunja kanuni za kitamaduni kwa kutaka kutoa talaka, jambo ambalo haliendani na itikadi za jamii hiyo.

Mume kuwa na wake wengi ni mojawapo ya masuala yanayokubalika katika jamii ya Wazulu, lakini Mfalme Misuzulu kaZwelithini amefanya uamuzi ambao sio wa kawaida kwa kuwasilisha kesi mahakamani ya kutaka kumtalaki mke wake wa kwanza, Malkia Ntokozo kaMayisela.

“Kila mmoja ameshangazwa. Watu hawakutarajia kwamba yangefikia kiwango cha kutaka kuotoa talaka,’ alisema Profesa Gugu Mazibuko ambaye ni mtaalamu wa utamaduni katika chuo kikuu cha Johannesburg huko Afrika Kusini.

‘Katika utamaduni wa jamii ya Wazulu, hakuna talaka. Haupaswi kumfukuza mke wako,’ alisema.

Mfalme wa Jamii ya Wazulu anayefahamika kama ‘Simba wa taifa,’ ndiye mwenye kuhifadhi tamaduni za jamii hii ambazo ni za jadi. Tamaduni hizi zimedumisha ndoa na hususan ndoa ya wake wengi kama jambo kubwa kabisa la mafanikio ya ufalme.

Na japo majukumu yake nchini Afrika Kusini ni ya kitamaduni na hayana uzito katika sheria za nchi hiyo, kiongozi huyu wa jamii anasalia kuwa na ushawishi mkubwa katika jamii huku ofisi yake ikipokea ufadhili wa mamilioni ya dola za Kimarekani kutoka kwa serikali kuu.

Mfalme huyo ambaye alikulia katika taifa jirani la Eswatini , alipata masomo yake nchini Marekani na kukabidhiwa wadhifa wa uongozi mnamo 2021. Aidha amekuwa akikabiliwa na utata tangu awali.

Kukabidhiwa kwake mamlaka kulipingwa mahakamani na kaka yake mkubwa ñ ambaye ni wa mama mwingine ñ aliyetaka kupokezwa ufalme huo.

Ndoa yake ya pili, imegonga vichwa vya habari, na jaribio lake kuoa mke wa tatu limegongwa mwamba huku kukiwa na ripoti kwamba ana uhusiano kwa kando na mwanamfamle wa kike.

Hata hivyo, kashfa inayozunguka maisha ya kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 50 imekuwa ikijadiliwa chini kwa chini ñ hadi pale alipotangaza azma ya kumtalaki mke wake na kuwasilisha ombi rasmi mahakamani mwezi Desemba.

Profesa Madibuko amekiri kwamba kumbukumbu za historia ya Wa Zulu zinaonyesha kwamba kuna mfalme ambaye katiak karne ya 20 alimtalaki mmoja wa wake zake , ’ ila hilo lilifanyika kimya kimya na kuwa siri kubwa katika familia hiyo ya kifalme,’ ikizingatiwa kwamba talaka katika ufamle wa zulu sio jambo la kawaida.

‘Ikiwa uhusiano utavunjika, basi mke huyu ataendelea kuishi katika boma la mfalme. Atapewa eneo lake kando, na hatakuwa na uhusiano an mfalme , ila yeye na watoto wake watatunzwa.’

Mama Myeni na Mfalme Misuzulu KaZwelithini. Chanzo cha picha,KwaZulu-Natal

Maelezo ya picha,Mfamle huenda ameahirisha ndoa yake ya mke wa tatu Nomzamo Myeni, ila wapenzi hao walionekana pamoja katika hafla ya kitaifa.

Ilikuwa muda kabla ya kupokezwa ufalme ñ punde tu baada ya kifo cha ghafla cha baba na mama yake miaka minne iliyopita ñ kwamba mwanamfalme (wakati huo) Misuzulu alipomuoa Ntokoto Mayisela.

Wawili hao walikuwa tayari kwenye uhusiano wa kimapnenzi na walikuwa tayari ni wazazi wa Watoto wawili , ila kwa mujibu wa mtaalamu mwingine wa utamaduni wa jamii ya Zulu, Prof Muza Xulu kutoka chuo kikuu cha Zululand, uamuzi wa kufunga ndoa ulionekana kuharakishwa.

‘Ilionekana kwamba mwanafalme hangeweza kuwa mfalme ikiwa hakuw ana mke,’ alioambia BBC.

Malkia kaMayisela alitokea familia ya kawaida ñ kama wake wengine wa wafalme wa Kizulu ñ kutoka mji mdogo wa uchimbaji madini katika jimbo la KwaZulu ñ Natal.

‘Malkia alimvutia Mfalme katika mgahawa mmoja kwenye mji wa pwani wa Durban alipokuwa akifanya kazi kama muimbaji,’alisema Prof Xulu.

Hadhi yake katika familia iliwekwa wazi wakati wa kutawazwa kwa mfalme mnamo Desemba 2022 alipoketi kando yake.

Ila nafasi yake sasa inatishika , anapotaja Mume wake kwamba wawili hao hawajaishi pamoja kama mume na mke kwa mwaka mmoja uliopita na kwamba ndoa yao imevunjika.

Kasri ya mfalme ilifuatilizia matamshi yake kwa kutuma mualiko wa ndoa ya Mfamle kwa mke mwingine, Nomzamo Mayeni mwishoni mwa mwezi Januari . Mahari ya bibi harusi inayofahamika kama LOBOLA kwa lugha ya kizulu imeshalipwa ñ huku ng’mbe wanaothaminiwa sana katika jamii hiyo wakitolewa kama mahari.

Malkia kaMayisela hajapokea haya yote vyema, akitaja kwamba huenda akawasilisha malalamishi ya kutaka ndoa hiyo kutofanyika , hali iliyosababisha ndoa hiyo kuahirishwa.

Ameiambia mahakama kwamba , mfalme ambaye anatambulika miongoni mwa jamii hiyo kama “ingonyama”, kumaanisha simba, angekuwa anavunja sheria za ndoa kwa kufunga ndoa ya pili japo mke wa kwanza yupo. Anasema pia kwamba hatua hiyo inafanyika chini ya ndoa iliyofanyika katika ofisi ya mwanasheria mkuu ambayo haikubaliwi kuwa na wake wengi na kwamba kabla

>> Itaendelea toleo lijalo...



JAMVI LA HABARI
SPOTI
JUMATANO MACHI 05, 2025



Kiba agoma kufanya interview Wasafi Tv

>> Soma Uk. 15

# SIMBA NA YANGA ZAJICHIMBIA DAR




NA SUSAN CHIRWA

KWA kawaida mambo yaliyokuwa yakitarajiwa huko nyuma kila inapokaribia mechi kubwa inayozikutanisha timu kongwe za Simba na Yanga, wachezaji, viongozi hulikimbia Jiji la Dar es Salaam na kwenda nje kwa ajili ya kufanya maandalizi.

Mara nyingi Simba ilishuhudiwa ikikimbilia Kisiwani Zanzibar na Yanga mara chache ilikuwa ikielekea Kisiwani Pemba au mikoa ya karibu na Dar es Salaam, Morogoro au Bagamoyo mkoa wa Pwani.

Lakini kadri siku zinavyozidi kwenda utaratibu huo umekuwa ukiondoka polepole na hivi sasa timu hizo zimekuwa zikisalia katika Jiji la Dar es Salaam huku kila timu ikijifua kambini kwake.

Inadaiwa kuwa utaratibu wa kuzitoa timu nje ya Jiji umekuwa ukipotea polepole kutokana na mabadikiko ya benchi la ufundi na hata wachezaji wa kigeni ambao wamekuwa wakishinda kuelewa mantiki yake.

Inadaiwa kuwa safari ya kuzitoa nje ya Dar timu hizo mara nyingi zilikuwa zikihusishwa na masuala ya ushirikina ambayo kwa sasa yanazidi kupoteza mvuto ndani ya klabu hizo.

## Wasemaji Simba, Yanga wafungwa midomo

NA MWANDISHI WETU

ZILE kejeli pamoja na tambo zilizozoeleka kusikika kila inapokaribia mechi ya watani wa jadi Simba na Yanga katika hali isiyokuwa ya kawaida zimezimika huku mashabiki wakibaki ndiyo wanaoendeleza majibizano vijiweni.

Habari ambazo gazeti hili limezipata zimedai kuwa ukimya huo umetokana na Maafisa wa Habari wa Klabu hizi Ahmed Ali wa Simba na Ali Kamwe wa Yanga kuitwa na Kamati ya Nidhamu ya Shirikisho la soka Tanzania TFF.



Hata hivyo Waandishi wa habari waliofuatilia taarifa hizo hawakupata majibu baada ya Wasemaji hao kutoka katika kikao hicho na kukataa kuzungumza chochote kilichojiri.

Uchunguzi wa gazeti hilo umebaini kuwa pamoja na mambo mengine huenda wanahabari hao waliopewa majukumu ya kuzizungumzia klabu hizo kubwa, wamepigwa pini kutokana na mara nyingi kukiuka miiko pale wanapozinadi timu zao, hasa kuelekea mchezo wa 'Derby' hiyo maarufu ukanda wa Afrika Mashariki.



## Guardiola ampigia hesabu Straika wa Uingereza

HAKUNA ubishi kuwa Kocha wa Manchester City Pep Guardiola ana mpango kabambe wa kuboresha kikosi chake, hivyo jambo la muhimu kwake ni kuhakikisha anasajili nyota watakaoweza kuvaa uhusika.

>> Inaendelea Uk. 14

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM